**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS-TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO**

***MAWASILIANO:***
***SIMU NAMBA: 0762 738564 AU 0764 921641***

SHULE YA SEKONDARI UDZUNGWA
S.L.P 1693
IRINGA
TAREHE……………………

Jina la mwanafunzi:……………………………………………………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI UDZUNGWA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO MKOA WA IRINGA MWAKA 2022.**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2022 tahasusi ya …………. Shule ya Sekondari Udzungwa. Shule hii ipo umbali wa Kilometa 58 Kusini Mashariki mwa mji wa Iringa. Ili kufika shuleni panda Basi la Mwafrika liendalo Idete au Bomalang'ombe au Basi la Upendo nauli ni Tsh. 3,000/=. Mabasi hayo yote yanaanzia safari zake stendi ya mabasi ya Mlandege Iringa mjini. Muda wa mabasi kuondoka Iringa mjini ni saa sita kamili mchana. Kituo cha kushuka ni Ifuo kwenye kibao cha Shule ya Sekondari Udzungwa. Umbali kutoka kituoni ni Kilometa 2.2 hadi shuleni.
NB: Nauli ya bodaboda kutoka kibao cha shule mpaka shuleni ni sh.3,000/=.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **05/09/2022** siku ya Jumatatu. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **28/08/2022** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **04/09/2022**.

## 2. HALI YA HEWA

**Shule ipo katika safu ya milima ya Udzungwa. Hivyo hali ya hewa ni baridi, ambayo ni nzuri kwa mwanafunzi kujisomea. Hata hivyo mwanao aje na blanketi zito na sweta zito lenye rangi nyekundu (pull over) lenye kofia kwaajili ya kuvaa muda wa kujisomea jioni/usiku.**

### 3.1 Sare ya shule

I. Sketi ya bluu bahari, ndefu inayovuka magoti yenye marinda nane (nne mbele na nne nyuma).
II. Mashati mawili meupe mikono mirefu.

III. **Suruali pana rangi ya sketi, nusu kanzu inayofika kwenye magoti na hijabu nyeupe inayofunika kifua. Hii ni kwa waislamu tu.**
IV. Tai inayofanana na rangi ya sketi (inapatikana shuleni shilling 3,000/=
V. Sweta rangi ya maziwa (cream) inapatikana shuleni shillingi 14,000/=
VI. Soksi nyeupe jozi mbili
VII. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba visivyo na kisigino kirefu

**3.2 ADA NA MICHANGO YA SHULE**

| | **MAHITAJI** | **KIASI** |
|---|---|---|
| 01 | Ada ya shule | 70,000/= |
| 02 | Mchango wa taaluma | 20,000/= |
| 03 | Mchango wa vibarua (walinzi, wapishi na wahudumu) | 30,000/= |
| 04 | Ukarabati | 20,000/= |
| 05 | Huduma ya kwanza | 10,000/= |
| 06 | Michezo | 5,000/= |
| 07 | Tahadhari | 5,000/= |
| 08 | Kitambulisho na picha | 6,000/= |
| 09 | Nembo ya shule | 2,000/= |
| 10 | Bima ya afya. | 5,000/= |
| 11 | Umeme na maji | 15,000/= |
| | **Jumla** | **188,000/=** |

Ada (Tsh 70,000/=) ilipwe kupitia Akaunti Namba **62301200031 NMB. Jina la Akaunti: Udzungwa Secondary Schoo**l.
Michango mingine yote (Tsh 118,000/=) ilipwe kupitia Akaunti namba **62302300243 NMB Jina la Akaunti: ELIMU YA KUJITEGEMEA UDZUNGWA SEKONDARI.**

**ZINGATIA:**

I. Hakuna fedha yoyote itakayopokelewa mkononi au kwa njia nyingine yoyote tofauti na benki.

II. Unapolipa hakikisha unaandika jina la mwanafunzi kwenye karatasi ya benki ya malipo (Bank pay in slip).
III. Ada kwa mwaka ni Tsh. 70,000/=. (Mzazi anaweza kulipa ada kwa mihula miwili yaani Tsh. 35,000/= kwa muhula wa kwanza na Tsh. 35,000/= kwa muhula wa pili).

**3.3 Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni**.

I. Godoro 3x6 inchi (5 unene)
II. Mashuka mawili (2) rangi ya pinki
III. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko n.k)
IV. Nguo za kazi (shamba dress) sketi dark bluu (bluu nyeusi ) marinda box mbele na nyuma, t-shirt inapatikana shuleni kwa bei ya shillingi 10,000/=. **NB: Kwa waislamu sketi dark blue ndefu mpaka chini(mpaka kwenye vifundo), Hijabu au mtandio rangi ya bluu bahari vifunike kifua.**
V. Track suit pana nyekundu jozi mbili kwa ajili ya michezo. Track suit aina ya Baloteli (inayobana chini) hairuhusiwi.
VI. Raba za Michezo jozi moja
VII. **Cheti cha kuzaliwa na vyeti vya kidato cha nne (Result slip na leaving certificate).**
VIII. Ream za karatasi 02(kwa mwaka)
IX. Vitabu vya masomo kwa tahasusi husika
X. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia
XI. Scientific calculator
XII. Laboratory coat kwa mwanafunzi wa CBG
XIII. Mathematical set
XIV. Taa ya kuchaji kwa jua (solata) 1
XV. Advanced learners Dictionary kwa wanafunzi wa HGL, HKL na HGK
XVI. Counter books kubwa za kutosha angalau kuanzia 10.
XVII. Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko kwa ajili ya matumizi ya mwanafunzi mwenyewe.
XVIII. Kwanja, jembe, mfagio mgumu na wakudekia(hard broom and dry broom).

**SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

**1. MAHUDHURIO**

Mwanafunzi anatakiwa kuwepo mahali anapotakiwa kwa mujibu wa taratibu na maelekezo atakayopewa na uongozi wa shule.

a) Kushiriki kukimbia mchakamchaka saa 11:30 hadi saa 12:00 alfajiri.
b) Kushiriki shughuli za usafi wa mazingira na usafi binafsi mara baada ya mchakamchaka.
c) Kuwahi mstarini mara tu kengele inapogongwa (saa 1:00 hadi saa 1:30 asubuhi) kila siku za masomo.
d) Kushiriki kazi zote za mikono.
e) Kuhudhuria mikutano yote ya shule mfano: Baraza la shule, midahalo, dini n.k.
f) Kuitikia miito ya dharura mara moja.

**2. HESHIMA**

a) Kuwathamini na kuwaheshimu wanafunzi wenzake wote wakubwa kwa wadogo.
b) Kusimama na kusalimu walimu au mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita au Kuingia mahali ulipo na kumpokea.

c) Kutumia lugha nzuri wakati wote.
d) Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.
e) Kuitika wito mara moja na kukimbia aliko aliyekuita.
f) Kushirikiana na wanafunzi wenzako wote katika masomo na kazi zingine.
g) Kuheshimu Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa vyama, serikali na Nembo ya Taifa , Wimbo wa Taifa, Wimbo wa shule na fedha za Taifa.
h) Kuheshimu vikao, ofisi za shule, mali binafsi na za umma.
i) Kunyoosha mkono kabla ya kujibu swali unapoulizwa unapokuwa darasani
j) Kukaa kimya darasani na mahala pengine popote penye mkusanyiko
k) Kutoka nje ya darasa kwa ruhusa ya mwalimu
l) Huruhusiwi kutumia madawa ya kulevya kama vile bangi, pombe au sigara ndani na nje ya shule.
m) Huruhusiwi kugombana, kutukana au kupigana.
n) Huruhusiwi kushiriki uasherati, wizi au utapeli.
o) Huruhusiwi kutoka nje ya shule bila kibali maalum (kibali kinapatikana ofisi ya Makamu mMkuu wa shule)
p) Huruhusiwi kutembelea nyumba za watumishi ,maabara na ofisi ya shule bila ruhusa maalum.
q) kuwa mfano mzuri wa kuigwa uwapo ndani na hata nje ya maeneo ya shule.
r) Huruhusiwi kabisa kutembelea:
    i. Vilabu vya pombe na baa
    ii. Majumba ya starehe.
    iii. Majumba ya kufikia wageni.
s) Mwanafunzi haruhusiwi kutembea eneo la paredi (Smart area).

**3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

I. Wizi
II. Uasherati, ubakaji, ushoga, ulawiti na usagaji.
III. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, biashara ya madawa yote ya kulevya.
IV. Makosa mengine ya jinai.
V. Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake, au mtumishi.
VI. Kuharibu mali ya umma na ya watu wengine
VII. Kudharau Bendera ya Taifa, Picha za viongozi wa Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
VIII. Kuoa au kuolewa
IX. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
X. Kutoa au kushawishi kutoa mimba.
XI. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.
XII. Kukataa adhabu halali.
XIII. Kujiachisha shule mwenyewe.

**4. SARE**

Unapaswa kuwa ndani ya sare ya shule zilizokubaliwa na kwa wakati kwa kadri utakavyoelekezwa:

a) Wakati wa masomo
b) Safari nje ya shule na kwa jina la shule

c) Kuwa na nguo za michezo wakati wa michezo na nguo maalum za kazi za nje (shamba dress).

**Mwisho:** Mzazi anashauriwa kumpeleka mwanae kupimwa na kujaziwa fomu iliyoambatanishwa na maagizo haya. Ni kosa kujijazia fomu hiyo.

*Tunakutakia maandalizi mema.*
**DOKEZO:** Tafadhali soma kwa makini maelekezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

***MOTTO WA SHULE:***
**"Fruits are sweet while roots are bitter''**

***KARIBUNI SANA UDZUNGWA SEKONDARI***

ASHERI MBOGORA MANYAMA
MKUU WA SHULE

**FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI**

**(B) HABARI ZA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili (kama kwenye vyeti vya mtihani)
   ……………………………………………………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa…………………… Dini ……………………………..
3. Mahali na Wilaya aliyozaliwa ………………………………………..
4. Shule aliyomaliza kidato cha nne …………………………………….
5. Masomo anayopendelea i. ……………………… ii. …………………
6. Kazi yoyote aliyowahi kuifanya kama vile kiongozi wa michezo, kwaya, ngoma, kiranja, maktaba n.k.
7. Mambo anayopendelea kufanya nje ya masomo (kama Michezo, ushonaji n.k)
8. Ninathibitisha kwamba habari zilizotolewa ni kweli na sahihi.

Jina la mwanafunzi ………………………………. sahihi …………………………….
Tarehe ……………………………………………………………………

**B. HABARI ZA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili la Baba ……………………………… yupo hai / amefariki
2. Kazi yake …………………………………………………………………
3. Jina kamili la mama ……………………………. Yupo hai / amefariki
4. Kazi yake ………………………………………………………………….
5. Jina kamili la mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake)
……………………………………………………………………………….
6. Kazi yake …………………………………………………………………..
7. Namba ya simu ya mzazi / mlezi ……………………………………..
8. Anuani ya mzazi / mlezi ………………………………………………
9. Mtoto anaishi na (i) Baba (ii) Mama tu (iii)wazazi wote (iv) Mlezi (kata lisilohusika)
10.Taja ndugu sita wa karibu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi awapo shuleni.

| NA | JINA | NAMBA YA SIMU/ANWANI | UHUSIANO |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |

11. Mimi ……………………………. Mzazi / mlezi wa ………………………………….
Ninathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na naahidi Kushirikiana na walimu kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri na mwenye bidii ya masomo.
Jina la mzazi /mlezi ……………………………….  sahihi ………….tarehe ………

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

To the medical in charge of ………………………………… Government hospital. Please examine the above named student as to his/her fitness for further studies.

Name ……………………………………………………………………………….

Blood count (red and white) ……………………………………………………….

Urine examination …………………………………………………………………..

Stool examination …………………………………………………………………..

Syphilis test ……………………………………………………………………………….

T.B test ……………………………………………………………………………………….

Ear test ……………………………………………………………………………………….

Eye test ………………………………………………………………………………………

Spleen test ……………………………………………………………………………….

Abdomen ……………………………………………………………………………………

Additional information of any other physical, mental, hereditary or infectious disease.

…………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………..

(Please state nature of treatment)

**MEDICAL CERTIFICATE:**

I certify that the above mentioned girl/boy has been examined and found fit/not fit to pursue A-Level studies.

Signature ……………………………………………………………………………….

Designation ……………………………………………………………………………..

Station ……………………………………………………………………………………

Date ……………………………………………………………………………………..…